**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA**

*Unapojibutafadhalitaja:*

**Kumb.Na.MODC/AD/PF.10/38VOL II/36** 15.08.2023

Kuh: **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba anayofuraha kutangaza nafasi 2 za ajira ya kudumu kwa watanzania wote wenye sifa stahiki katika nafasi ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III.** Nafasi za ajira hizi zinatokana na kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora kwa barua yenye **Kumb. Na:FA.170/571/0"A"/54** cha tarehe **26/06/2023.**

MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III – Nafasi 2

SIFA ZA MWOMBAJI;

- Mwombaji awe Raia wa Tanzania.
- Awe na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18.
- Awe amehitimu mafunzo katika ngazi ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambulika na Serikali.
- Maombi yote yaambatishwe na Nakala ya cheti cha Taaluma, Nakala ya cheti cha Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI), Maelezo binafsi yanayojitosheleza (CV) ikiwa na anuani, namba ya simu za kuaminika na picha mbili (Passport size) za hivi karibuni (ziandikwe majina kwa nyuma).
- Vyeti vyote vya Taaluma na Kidato cha Nne (IV) / Sita (VI) ni lazima visibitishwe na Hakimu au wakili anayetambulika na Serikali. Aidha atakayewasilisha taarifa na sifa za kughushi atachukuliwa hatua za Kisheria na mamlaka zinazohusika.
- Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu maombi yake hayatashughulikiwa.

*OfisiyaMkurugenziMtendaji (W), Chitete – Momba, S. L. P 273,TUNDUMA – MOMBA – SONGWE*
*Barua pepe ded.mombadc@go.tz, Tovuti: http://www.mombadc.go.tz/*
*Simu Na. 0252954102, Fax Na. 0252954102*

**KAZI/ MAJUKUMU**

i. Afisa Masuuli ni Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu za Serikali katika Kijiji.
vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalamu katika Kijiji.
viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
ix. Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
x. Kupokea, kusikiliza kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
xi. Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji.
xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

Mshahara;
*Ngazi ya Mshahara wa Serikali TGS B*

3. Ifahamike kuwa watakaoitwa kwenye usaili ni wale tu waliokidhi vigezo vilivyowekwa.

4. maombi yote yatumwe kwa njia ya posta, yatakayowasilishwa kwa mkono au barua pepe hayatafanyiwa kazi. ***Barua zote zitumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo;-***

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Momba,
S. L. P 273,
**MOMBA.**

5. Maombi yote yatumwe kuanzia tarehe 16/08/2023 mwisho tarehe 29/08/2023 siku ya Jumanne, saa 09:30 Alasiri.

Regina L. Bieda
**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOMBA.**

**Nakala:**
Kalibu Tawala (M),
S.L.P 23,
**SONGWE.**

Kalibu tawala (W),
S.L.P 273,
MOMBA.

Mbao zote za Matangazo,
Kata zote
Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Tunduma Mji.

*OfisiyaMkurugenziMtendaji (W), Chitete – Momba, S. L. P 273,TUNDUMA – MOMBA – SONGWE*
*Barua pepe ded.mombadc@go.tz; Tovuti: http://www.mombadc.go.tz/*
*Simu Na. 0252954102, Fax Na. 0252954102*